**Sikiliza na Ujifunze – Mazingira na Hali ya Hewa**
**10 – Seafood (Chakula kinachotoka Baharini)**
**Text: Richard Lough**
**Redaction und Idee: Johannes Beck**
**Translator: Mohamed Dahman**

---

Hujambo msikilizaji! Karibu katika mfululizo wa vipindi vya Sikiliza na Ujifunze ambavyo huangalia masuala ya mazingira. Leo hiii tutaangalia juhudi za kuokoa jamii ya viumbe hai baharini inayotishiwa sana kutoweka ya kasa na wale wenye kuwinda na kula samaki wenzao yaani papa. Kasa ni mnyama mtambazi wa zamani ambaye ameweza kunusurika asitoweke kama alivyotoweka dinosau mnyama mkubwa sana wa zama za kale mwenye umbo la kenge. Lakini bila ya kuchukuliwa kwa hatua ya dharura kuwahifadhi siku za kubakia kwao duniani zinakaribia kumalizika. Leo tutafahamu kwa nini ni muhimu kuwaelimisha wavuvi watumie nyavu za kuvulia zisizoleta madhara kwa kasa. Na tutagundua kwa nini zaidi ya jamii 100 ya papa inaweza kutokomezwa kwenye uso wa dunia hivi karibuni kwa sababu tu ya kikombe kimoja cha supu yao!

Na je ulikuwa ukijua kwamba kuna nyavu za kuvulia zenye ukubwa wa kuingiza dazeni moja ya ndege za aina jumbo. Richard Lough (anatamkwa Lock) mwandishi wa Radio Deutsche Welle nchini Kenya atatufahamisha vipi binaadamu wanatumia teknolojia ya kisasa kutokomeza akiba ya samaki baharini kufikia hatua ya kutoweka duniani.

**Music-0:30**

**SFX – Waves on beach…….Mawimbi ufukweni**

**Gladys:** Nilikuwa kwenye ufukwe huu jana usiku. Moses hebu agua niliona nini…

**Moses:** Uliona nini Gladys?

**Gladys:** (Excitement… tamka kwa msisimko) Kasa! Sasa ni msimu wao wa kutaga…

**Monica:** (Exlaims… toa sauti ya mshangao): Owww… Unajuwa nilikuwa nikiishi mwendo wa muda mfupi kutoka ufukwe huu maisha yangu yote na katu sikuwahi kumuona kasa akitaga mayai Lakini nakumbuka wakati tulipokuwa shule tulikuwa tukisika juu ya majangili wanaoiba mayai ya kasa. Na unaweza kuamini kwamba bado kuna watu wanaokula nyama ya kasa!

**Moses:** Bila ya shaka Monica… mimi nakula.

**Monica/Gladys:**(horrified… wakiwa wameshtuka) Ohh Moses!

**Moses:** Kwa sababu baba yangu anasema ni rahisi. Wavuvi huwa hawakusudii kuvua kasa lakini kasa hao malisho yao huwa katika maji yale yale walioko samaki kama vile kwenye matumbawe ambayo hayako mbali na fukwe. Siku nyengine kwa bahati mbaya wanakuja kunasa kwenye nyavu za wavuvi.

**Gladys:** Bila ya shaka lazima watanasa na baadaye hufa maji kwa sababu huwa wanavuta pumzi ya hewa kama mimi na wewe.

**Monica:** Siku hizi kuna uvuvi mkubwa unaofanyika kwenye bahari yetu na unaangamiza idadi ya kasa wetu. Moses unapaswa kususia nyama ya kasa.

**Moses:** Lakini kwa nini nisusie Monica? Iwapo kasa huyo amekufa kwa nini nisimle?

**SFX – Music from beach bar …sauti ya muziki kwa mbali kutoka baa ya ufukweni**

**John:** (calls out off mic… anaita kwenye kipaza sauti) Hee Gladys

**Gladys:** Naam John. Yule ni kaka yangu John, twendeni tukazungumze naye …

**Fade –up SFX – Music from beach bar …changanya kwa kupandisha sauti ya muziki kutoka baa ya ufukweni**

**Gladys:** Nilikuwa nikiwahadithia Monica na Moses juu ya wale kasa wa jana usiku.

**John:** (clap of the hand…… kupiga kofi) Ohh ilikuwa ni maajabu! Unajua mimi mwenyewe nilikuwa nikiwakamata kasa ilikuwa sio kusudio langu lakini wakati ule nilifikiri kuwa lilikuwa ni jambo lisiloepukika na nilikuwa nikiweza kujipatia fedha kidogo za ziada kwa hiyo nikaona kwa nini nilaze damu… nizubae.

**Monica:** Nini kilichokufanya ubadili mawazo yako?

**John:** Umewahi kusikia juu ya mpango wa kuhifadhi kasa? Huu ni mpango wa kuwaelimisha wakulima juu ya haja ya kuwatunza kasa. Nilikuwa sikuwaza kabisa kwamba idadi yao inatishiwa na harakati za wavuvi kama mimi. Niliona aibu kwa vitendo vyangu.

**Moses:** Lakini vipi unaweza kuepuka kuwanasa kwenye nyavu zenu ikiwa hiyo mnasema ni bahati mbaya?

**John:** Enhee njoo nikuonyeshe nyavu zangu …

**SFX – pushing chairs back .X-fade into SFX hammering**
**Kurudisha viti nyuma …. Changanya na saiti ya nyundo**

**Johnn: Vijana pale wanafanya matengenezo kwa mashua. Angalia hapa hizi ndio nyavu tunazozitumia hivi sasa.**

**SFX –hauling net out of boat …….kutowa nyavu nje ya mashua**
**SFX –tapping metal………..kugonga chuma**

**John:** Hiki tunakiita kuwa Kifaa cha Kutomuingiza Kasa. Ni kifaa cha chuma chenye matundu kinachowekwa kwenye mlango wa nyavu ya inayokokotwa na meli. Hii inamaanisha kwamba vitu vikubwa kama kasa haviwezi kupenya kwenye nyavu wakati samaki na uduvi huwa wanaweza.

**Monica:** Lakini kweli vinafanya kazi ipasavyo?

**John:** Ndiyo, katika baadhi ya sehemu za dunia ambapo vifaa hivi vinatumika sana idadi ya kasa wanaonaswa kwenye nyavu imepunguwa kwa hadi asilimia tisini.

**Moses:** John umewahi kuwanasa kasa walio hai?

**John:** Ndiyo… tumewahi.

**Gladys:** Na je wakati mlipowanasa mmewarudisha baharini?

**John:** Hapana. Inabidi nikiri kwamba tumewaua na kuwauza sokoni. Tuliona hiyo kama bakshishi. Lakini sasa nimepata mwamko na tumekuwa tukiwaambia wavuvi wengine kuwaachilia baharini kasa wanaowanasa. Lakini unajua tatizo hasa ni ujangili… mnajua nyie hapa kuna mtu nataka mkutane naye…

**SFX – knock on door… sauti ya kugonga mlango )**

**Peter:** Habari gani John …

**John:** Nzuri Peter… nataka nikujulishe na dada yangu Gladys na marafiki zake.

**Peter:** Hamjambo…

**Moses/Gladys/Monica:** Hatujambo Peter …

**Peter:** Karibuni! Je naweza kuwasaidia nini?

**John:** Nilikuwa naomba uwachukuwe ufukweni jioni hii na uwaonyeshe kasa wakitaga .Jana nilimpeleka Gladys kuona lakini wenzake katu hawakuwahi kuona.

**Peter:** Hakuna tabu … tukutane ufukweni saa tano usiku.

**SFX – night insects and SFX waves on the beach ….sauti ya wadudu wa usiku na mawimbi ya bahari…**

**Peter:** Haya… twendeni tukaangalie kasa…

**SFX - walking across sand……wakitembea katika mchanga**

**Peter:** (hushed exclaim… akizungumza kwa sauti ya chini) Angalieni pale …

**Moses:** Wapi?

**Monica:** Ahh pale pembezoni mwa jabali …

**Peter:** Ndiyo Monica. Kila mwaka mamia ya kasa wanakuja kutaga hapa. Daima huwa wanarudi kwenye ufukwe ule ule. Miaka mitano iliyopita majangili waliiba asilimia 95 ya mayai yaliotagwa hapa na kwa kiasi kikubwa kuyatumia kwa ajili ya chakula. Hivi sasa kutokana na mpango wa elimu tunaouendesha kumekuwa hakuna kabisa ujangili. Hebu tuwasogelee karibu kwa kutambaa…

**SFX crawling through sand …….wakitambaa kwenye mchanga**

**Gladys:** Kwani kasa mmoja huwa anataga mayai mangapi?

**Peter:** Mara nyingi huwa zaidi ya mia moja.

**Moses:** Kwa hiyo kuna ubaya gani ikiwa baadhi ya mayai hayo yatachukuliwa?

**Peter:** Hapana haifai kuchukuliwa! Kiwango cha kasa wanaoweza kunusurika kwa kuendelea kuishi kufikia umri wa kukutana kimapenzi ni cha chini mno. Ni kasa mmoja tu kati ya kasa elfu wanaoanguliwa ambao wanaweza kuingia baharini wanafikia umri wa utu uzima. Na halafu huchukua miaka 40 kufikia umri wa kutaga.

**Gladys:** Ndio maana ni muhimu sana kuwalinda kasa ?

**Peter :** Sawa kabisa Gladys. Je mnajuwa kwamba jamii sita ya kasa kati ya saba walioko katika bahari duniani wamewekwa kwenye orodha ya wanaotishiwa au walioko hatarini kabisa kutoweka? Haya sasa na turudi……

**SFX – walking across the sand …wakitembea kwenye mchanga**

**Monica:** Hivi karibuni katika darasa la sayansi nimejifunza kwamba baadhi ya jamii ya papa pia wako kwenye orodha ya wanaotishiwa kutoweka duniani.

**Peter:** Ni sawa Monica. Binaadamu wanawamaliza papa baharini na iwapo tutaendelea na mwenendo huo kuna hatari kubwa ya kutoweka kwa baadhi yao katika kipindi cha miongo michache ijayo.

**Moses:** Lakini je tunapaswa kujali… kwani kwa vyovyote vile papa wanakula watu…

**Monica:** Hapo ndipo unapokosea Moses! Kwa kweli mara nyingi mashambulizi ya papa dhidi ya binaadamu yanakuwa ni makosa ya kutambua. Hii ni kusema papa hao huwa wanawadhania kwa makosa binaadamu walioko majini kuwa ni mawindo yao ya

kawaida ya kama vile sili mnyama wa baharini mwenye manyoya.

**Peter:** Barabara kabisa! Na katika kujibu swali lako Moses: ndiyo tunatakiwa kujali kwani hivi sasa kuna jamii 126 ya papa walioanishwa kuwa wako kwenye hatari ya kutoweka.

**Gladys/Moses:** **(**Exclaim… kwa sauti ya mshangao) Hee… kwa nini wengi hivyo?

**Peter:** Idadi ndogo ya papa huvuliwa nje ya fukwe zetu. Utaweza kuona papa wakiuzwa kwenye masoko yetu na huwa rahisi kulinganishwa na samaki aina nyingine lakini unatakiwa ugome kumnunua.

**Monica:** Tumesikia kwamba tishio kubwa kabisa linalowakabili papa ni soko la supu ya pezi la papa huko kusini mwa Asia.

**Peter:** Hasa! Inakadiriwa kwamba papa milioni 40 huuwawa kila mwaka kutokana na mapezi yao ambayo huwa na bei za juu katika maakulati ya jioni huko Asia.

**Moses:** (Exclaim - sauti ya mshangao) Milioni 40!

**Peter:** Baadhi ya wanaharakati wa kutunza mazingira wanasema idadi hiyo inaweza hata kufikia milioni 100. Siku nyengine huwa wanakata mapezi ya papa na mikia yao wakati bado wangali hai kabla ya kuwatupa tena baharini kuwaacha wafe taratibu kifo cha mateso makubwa.

**Monica:** Iwapo papa ni mnyama mkubwa mwenye kuwinda na kula samaki wenzake baharini inakuwaje tena jambo hilo kuathiri mfumo wa ekolojia wa samaki mkubwa

kumla mdogo na mdogo kumla mduchu na kadhalika?

**Peter:** Naam… iwapo idadi ya samaki kama vile jodari na taa itaongezeka bila ya kudhibitiwa itaangamiza jamii ya samaki wadogo wadogo. Papa ni simba na duma wa bahari iwapo tutawapoteza kutakuwepo na uharibifu wa muda mrefu kwa mfumo wa ekolojia baharini.

**Music: 0:30**

**Je ulikuwa ukijua ?**

Je ulikuwa ukijua kwamba tunawamaliza samaki walioko baharini duniani? Ukweli juu ya uvuvi wa kisasa ni kwamba ulimwengu wa shughuli hizo za uvuvi umetawaliwa na meli za uvuvi ambazo hazilingani kabisa na uwezo wa maumbile ya asili kushehena tena samaki. Meli kubwa za uvuvi hutumia maarifa ya chombo cha sona chenye kugunduwa vitu vya chini ya maji cha kutafuta samaki ambacho kinaweza kuonyesha wapi walipo mkururo wa samaki kwa haraka na kwa usahihi kabisa. Kwa ufupi samaki wanakuwa hawana nafasi kabisa ya kukimbia.

Hapa tuna baadhi ya ukweli wa kufadhaisha kutoka kwa kundi la kutetea mazingira la Greenpeace. Kwanza kabisa samaki na viumbe wengine wanaonaswa kutoka baharini idadi yao imeongezeka mara nne zaidi katika kipidni cha miaka 50 kutoka tani milioni 18.5 katika miaka ya 1950 hadi kufikia tani zaidi ya milioni 80 hii leo. Kama matokeo aina saba kati ya nane ya samaki wanaovuliwa kibiashara baharini kama vile jodari na chewa wanavuliwa kupindukia kikomo cha usalama wa ekolojia.

Je vipi jambo hilo linawezekana? Ndiyo, angalia nyavu kubwa kabisa ya uvuvi. Ni kubwa kabisa kiasi kwamba inaweza kuzingira dazeni moja ya ndege za aina ya jumbo. Mzingo wa nyavu hiyo una kipimo cha kufadhaisha cha kilomita mbili.Meli zenye kutumia nyavu za aina hii zinaweza kuvuwa takriban tani kumi za samaki kwa saa. Lakini

uvuvi wa kiwango hiki huwa unafanyika kiholela.Inafikiriwa kwamba karibu theluthi moja ya samaki hao hawafikishwi kwenye masoko …. idadi hiyo ni kama sawa na tani 27 milioni za samaki wasiotakikana ambao hutupwa baharini wakiwa wamekufa. Hivi sasa meli za uvuvi duniani zinavuwa samaki kwa kukokota wavu chini katika bahari za kimataifa… zisizomilikiwa na mataifa kutafuta maeneo mapya ya samaki.

Mamilioni ya wanyama wengine ziada ya samaki wanajeruhuwa vibaya sana au kuuwawa kutokana na uvuvi wa biashara. Mamilioni ya pomboo wamekufa kwenye nyavu zinazotumika kuwanasia samaki wa jodari wakati maelfu ya ndege wa pwani jamii ya albatros wanauwawa kila mwaka na meli zenye kutupa mishipi yenye maelfu ya ndoana katika kilomita nyingi baharini.

Makundi ya kutetea utunzaji wa mazingira yanalaumu mataifa makuu 20 ya uvuvi ambayo huvua asilimia 80 ya samaki badala ya wavuvi wadogo wadogo. Hata hivyo wanasema jibu kwa ufumbuzi wa tatizo hilo ni rahisi: vua samaki wachache na ruhusu akiba ya samaki irudi kwenye hali yake ya kawaida. Lakini ulimwengu wa uvuvi wa samaki hauonyeshi dalili za kupunguza shughuli zao.

**Outro…… Funga kipindi**

Na hapo ndio tumefikia mwisho wa mfululizo wa vipindi maalum Sikiliza na Ujifunze juu ya mazingira kilicholenga wanyama wa baharini walioko hatarini kutoweka. Usile nyama ya kasa na usifanye ujangili wa mayai ya kasa iwapo unataka kuwasaidia wanyama hawa watambazi ambao wamenusurika kutoweka kama walivyotoweka dinosau wanyama wenzake wa enzi ya kale wenye umbo kubwa sana la kenge.

Ahsante kwa kujumuika nasi iwapo unataka kukisikiliza tena kipindi hiki au kuwaelezea marafiki zako nenda kwenye mtando wetu www.dw-world.de/lbe.
Kwa heri.